

Wazin wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) akipata maelezo kutoka kwa mkaano rasasi ya Afafasafe na mafuta mazito yataokolewa kutokana na mradi huo ambao unategemea kuanza wakati wowote kuanzia sasa. Na Mpigapicha Wetu umeme kutoka Makambako hadi Songea wakati akitaguzi utekelezaji wa mradi huo ambao tayari umekamilika. Zaidi ya shilingi billioni 9.1 za mafuta mazito yataokolewa kutokana na mradi huo ambao unategemea kuanza wakati wowote kuanzia sasa. Na Mpigapicha Wetu

Taasisi ya jipanga kuzalisha dawa ya kuuwa wadudu

Na Penina Malundo

■■■ TAASISI ya Kimataifa ya Klimo cha Kitropiko (ITA), ina mkakati wa kuanza kuzalisha dawa aina ya Afafasafe ya kuuwa wadudu wanaotokana na mazao ya nafaka, ikiwemo mahindi na karanga ili kuepukana na gharama za kuagiza nje ya nchi.

Akizingumza Dar es Salaam juzi Mkurugenzi wa Shirika la Dalberg Global Development Advisors and Chemonics, Steve Kisakyé wakati wa mikutano wa wadau wa kujadili jinsi ya kuanzisha dawa hiyo, ambayo itakuwa mkombozi kwa wakulima.

Kisakyé alisema, dawa hizo zikianza kuzalishwa nchini zitapunguza gharama za kuagiza dawa nje ya nchi na pia zitasaidia wakulima kuzipata kwa wakati na urahisi, ikiwa ni pamoja na kuleta tija katika uchumi wa kati

wa viwanda.

"Kuagiza nje, dawa ni gharama, tutatengeneza hapa hapa nchini ili tuweze kuwafikia wakulima ambao ndio wahusika wakuu kwa wakati na kuleta tija katika uchumi wa viwanda," alisema Kisakyé.

Aliungeza kuwa sumukuvu ni ugonjwa mbaya, ambayo aina rangi, harufu wala ladha inajulikana kwa kuleta madhara kwa binadamu kama vile saratani ya ini na huingia mwilini kuititia njia ya chakula, pia ikwa nyinyi husababisha kifo.

Alisema, pia sumukuvu husababisha udumavu kwa watoto na kupunguza kinga za mwili, mifugo huathiriwa pamoja na kuathini soko la ndani na nje ya nchi.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Taasisi ya Kimataifa ya Klimo cha

Kitropiko (ITA), Dkt. Victor Manyong alisema Afafasafe imetengeneza kwa kutimiza fangas, au kuvu asilia jamii ya 11 ambayo hupatikana kwenye udongo na masalia ya karanga na mahindi shambari.

Alisema, Afafasafe ina mjumuiko wa fangasi wasio na uwezo wa kuzalisha sumukuvu, fangasi hao na kuwaondoa fangasi wanaozalisha sumukuvu hiyo husaidia kupunguza sumukuvu kwa asilia 80 hadi 90 katika mazao ya mahindi na karanga.

Wakati huo huo, Ofisa Klimo Mkuu kutoka Wizara ya Kilimo, Betrice Pallangiyo aliwashauri wakulima kuvuna mahindi ya lyokauka na kuyaanika kwenye maturubai, ili kuepukana na sumukuvu.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi ya Aflatoxin Technology Transfer and

Commercialization Initiative (aTTC), Abdou Konlambigue alisema kwa kutumia teknoloja hiyo Tanzania itajahikishia kuwa na chakula salama kwa matumizi ya ndani na kufika kwango hitajika cha usafirishaj wa mazao nje ya nchi.

Alisema, taasisi ya aTTC, imetengeneza mkakati wa kuwezesha teknoloja hiyo kuzalishwa kibashara kwa msaada wa kiufundi wa Shirika la Kimataifa la Dalberg Global Development Advisors and Chemonics.

"Mchakato wa kusajili teknoloja hiyo kwenye Mamlaka ya Taasisi ya Ukauzi na Udhibiti wa Viwatisi (TPRI), unakaribia kukamilika na huamishaji wa teknolojia kutoka ITA kwa ajili ya kuzalisha kwa wingi kuititia aTTC, ili wakukima wafaidike, alisema.